**Mhariri**

Nimewahi kusema mara nyingi juu ya malori yanayotakiwa kuondoka Mbezi saa 3:00 asubuhi yamekuwa yakiondoka kabla ya muda huo na kuleta usumbufu mkubwa.Nilidhani baada ya kulalamikia suala hilo mara nyingi askari wa usalama barabarani wangelichukulia suala hilo kwa makini na kuyazuia.

Nadhani wote tunafahamu utaratibu uliowekwa na mamlaka husika juu ya kuyasimamisha malori kila inapofika saa 11.00 alfajiri eneo la Mbezi kuwa yasiendelee na safari kwa lengo la kupunguza msongamano kwa magari madogo na mabasi ambayo mamlaka hiyo imeona ndiyo yenye umuhimu wa kuwahi asubuhi.

Kwa taratibu ninazofahamu mimi baada ya malori hayo kutakiwa kuegeshwa hadi inapofika saa3:00 asubuhi ndiyo yaanze kuruhusiwa tena naona kama ni suala ambalo halitiliwi maanani.

Mwazo kabisa utaratibu huo ulionekana kuwa unafuatwa , lakini jinsi siku zinavyoenda tunaona hayafuati utaratibu huo tena .Ulegezaji wa tabia hiyo umeanza kidogo kidogo ambapo mwazo yalikuwa yakiondoka kabla ya saa tatu kasoro dakika kumi au kumi na tano .

Lakini sasa hivi malori mengi

**MJADALA**

# Kwanini mazingira ya kuanzisha biashara bado ni magumu?

Na Badru Kimwaga

MAZINGIRA ya uwekezaji Tanzania yameendelea kuwa magumu kulinganisha na nchi mbalimbali duniani na hiyo ikitokana na masuala kadhaa kama rushwa, tatizo la barabara na urasimu,Mwandishi Wetu amezungumzia utafiti uliofanywa na taasisi moja hapa nchini pamoja na wadau kadhaa wa hapa nchini kuhusu namna ya kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji.

Kampuni ya BEST- AC ilifanya utafiti kuhusu mazingira ya ufanyaji wa biashara nchini ambapo viongozi wa biashara waliulizwa juu ya mambo muhimu yatakayoleta mazingira mazuri kwenye biashara zao, Vituvinavyofanya biashara yao iwe ngumu,Vikwazo visivyokuwa vya kodi ambavyo ni muhimu kwenye biashara zao na vikwazo visivyokuwa vya kodi vinavyoleta matatizo kwenye biashara zao.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwezeshaji), Dk. Mary Nagu

iwapo serikali inafanya jitihada yoyote katika kushughulikia kila moja ya

wa Ufanyaji Biashara (Doing Business)

Benki ya Dunia hufanya tafiti mbalimbali kuangalia vipengele mbalimbali kisha huvichapisha kwenye ripoti kila mwaka kwenye ripoti inayojulikana kama "Doing Business"

Ripoti ya Doing Business 2012, iniaweka Tanzania kwenye nafasi ya 127, nafasi ambayo haitofautiani sana na mwaka jana. Kwa ukweli nafasi yake katika maeneo, muhimu yakufanya biashara yamebakia pale pale pia.

Pengine inaleta maana zaidi kama utalinganisha jitihada za Tanzania na nchi nyingine kwenye ukanda huu.. Rwanda ilishikanafasi ya kwanza kwa mwaka 2009 kulingana na ripoti yaDoing Business yamwaka 2010, ambapo ilipanda kwa nafasi 76; na kwa mwaka 2010 ilishika nafasi ya pili kwa kuleta mabadiliko, ambapo ilipanda kwa nafasi 9. Tanzania imebakia karibu pale pale

dekeza kuwa wafanyabiashara wengi watafurahi zaidi kulipa kodi na tozo mbalimbali kama mzigo wa kiutawala utapunguzwa vyakutosha na kama matumizi ya serikali yatakuwa ya wazi zaidi

Kiasi kikubwa cha mzigo wa kiutawala unatwishwa kwenye biashara zote kukamilisha nyaraka za leseni na kodi kwa mwezi , miezi minne na kwa mwaka.

Ukiachia mbali gharama halisi ambazo wafanya biashara wanalipa, gharama hizi za kiutawala zinajitafsiri kwenye gharama kutokana na ukweli kuwa muda inabidi utengwe kushughulikia—kuielewa sheria yenyewe, kuchukua fomu kuitoa kwenye mtandao (download), kujaza ,kuitolea nakala , kupata nakala za wakala wengine wa serikali, kuzijaza na kupata nyaraka nyingine za kuzithibitisha, kuziwasilisha kwenye ofisi mbalimbali za serikali , kuhakikisha kama zimefika nakuzifuatilia kwenye wakala husika za serikali.